OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI)

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

MKOA WA SIMIYU :

SHULE YA SEKONDARI MASANZA
S L P 157
BUSEGA.

Kumb. Na. MSS / A.1 /VOL I / 04

17 / 12 / 2021

MZAZI / MLEZI WA ……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2020

Ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanao ……. Amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari MASANZA.Ninampongeza kwa ushindi huo.

Shule ya sekondari MASANZA ni shule ya kutwa yenye lengo madhubuti la kuwapatia vijana elimu, na fikra zitakazo wafaa wakati watakapo ishi katika jamii inayokubalika.

Hatuna shaka kuwa atatumia nafasi hii kwani kuna wengi waliistaili lakini wameikosa.Tunaamini hataliangusha Taifa. Anatakiwa kuripoti shuleni hapa tayari kwa kuanza masomo tarehe 11/ 01 / 2021 na awe na cheti cha kuzaliwa

Tunakukaribisha sana shule ya sekondari MASANZA.Pamoja na barua hii nakutumia viambatanisho vifuatavyo :

i. Orodha ya mahitaji ya shule
ii. Fomu ya hospitali
iii. Sheria za shule
iv. Fomu ya taarifa binafsi ya wanafunzi

MWISHO: Hakikisha unakuja shuleni tarehe 011 / 01 / 2021 Kama ilivyopangwa. Hivyo usipofika shuleni tarehe iliyopangwa wala kutoa taarifa nafasi yako itachukuliwa na mtu mwingine.

Ni matumaini yangu kuwa utatumia nafasi hii kama ulivyotunukiwa na Taifa lako.

Karibuni sana,

…….

AZIZ .M. SALEHE

MKUU WA SHULE

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A) SARE ZA SHULE

I: MAVAZI YA DARASANI

1. Mashati meupe mikono mifupi wavulana na wasichana
2. Suruali mbili rangi nyeusi yenye upana wa inchi 18 chini kwa wavulana na wasichana sketi mbili rangi nyeusi nzito(RINDA BOX) ndefu kufikia kwenye jicho la mguu sketi fupi juu ya jicho la mguu haitakubaliwa.
3. Viatu vya ngozi rangi nyeusi visigino butu/soli fupi na viwe ni vya kufunga na kamba / gidamu
4. Soksi nyeupe ndefu kwa wasichana na fupi kwa wavulana
5. Tai yenye rangi ya nyeusi

II: MAVAZI YA MICHEZO

1. Aje na bukta za michezo kwa wavulana na wasichana na awe na track suit ya rangi ya blue
2. Viatu jozi moja (raba) kwa wavulana na wasichana
3. T.shirt/Jezi

C: VIFAA VINGINE

i) Daftari counter book zisizopungua 10

ii) Kalmu,penselii , rula, mkebe, dictionary ndogo ya kwako binafsikwa ajili ya kujifunza lugha ya kiingereza na begi la kubebea vifaa hivyo.

iii) SOFT BROOM na NDOO moja ndogo kwa wanafunzi wote, Fyekeo/slesha 1 kwa wavulana na Jembe 1 kwa wasichana.

SHERIA ZA SHULE

Sheria zote za shule zimewekwa ili kuwawezesha wanafunzi wote kuwepo shuleni bila matatizo, aidha sote tunaelewa kuwa NIDHAMU nzuri huambatana na mafanikio kitaaluma pia.

MAHUDHURIO

i. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie pale anapotakiwa bila kukosawala kuchelewa

ii. Ni lazima mwanafunzi awepo shuleni muda wote wa masomo

iii. Ni lazima kuzingatia siku za kufunga shule na kufungua shule

iv. Ni lazima mwanafunzi awahi na kushiriki shughuli zote na kushiriki katika shughuli zote za shule, kuitwa majina,usafi wa mazingira,shughuli za uzalishaji mali,michezo nk.Atakayechelewa na au kutohudhuria shughuli hizo ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria

v. Mwanafunzi atatakiwa kuitikia mara moja na kukimbia kuelekea mahali atakiwapo wakati asikiapo kengele au mwito mwingine wowote

vi. Utoro hautakiwi hapa shuleni,endapo mwanafunzi atabainika kuwa mtoro atahesabiwa kuwa hapendi shule na adhabu kali itatolewa kwa yeyote atakayekiuka agizo hili ikiwa ni pamoja na kuitaarifu bodi ya shule kwa uamuzi zaidi

vii. Ruhusa ya kwenda hospitali itatolewa na mwalimu wa zamu kupitia kwa mwalimu wa darasa Ruhusa ya kutoka au kuondoka shule kwa sababu ya shida nzito kama vile msiba itatolewa na mkuu wa shule ama makamu mkuu wa shule iwapo mkuu hatakuwepo

viii. Mzazi au mlezi aliye andikishwa shuleni ndiye atakayeruhusiwa kumwombea mwanafunzi ruhusa kila inapolazimu kufanya hivyo na si vinginevyo.

MIPAKA YA SHULE

Ni marufuku kutoka nje ya MIPAKA ya eneo la shule wakati wa masomo na shughuli nyingine za shule bila kuwa na ruhusa kutoka kwa walimu wanaohusika

MAKOSA MAKUBWA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i) Wizi
ii) Uasherati na ushoga
iii) Uvutaji bangi
iv) Kupigana na kupiga
v) Makosa ya jinai
vi) Kuharibu kwa makusudi mali za umma
vii) Kudharau bendera na wimbo wa taifa(pindi wakipandisha bendera na kuimba wimbo huo)
viii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
ix) Kuoa au kuolewa
x) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xi) Kupata ama kusababisha mimba ndani na nje ya shule
xii) Kupata ujauzito au kutoa mimba
xiii) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu
xiv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujmla.
xv) Kukataa adhabu kwa makusudi
xvi) Kumiliki au Kupatikana na simu ya mkononi katika mazingira ya shule

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

FOMU YA TAARIFA BINAFSIYA MWANAFUNZI YA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

A: TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

- JINA LA MWANAFUNZI……
- TAREHE YA KUZALIWA ……..(kama ilivyo katika cheti)
- MAHALI ALIPOZALIWA (MKOA , WILAYA) ……..
- MNAISHI/MNAKAA WAPI? MJI …..... KITONGOJI ……KIJIJI …… KATA…….
- MTANZANIA /SIO MTANZANIA ……

KUSAJIRIWA

- SHULE ULIYOTOKA ……
- NAMBA YA MTIHANI ……..

B: TAARIFA BINAFSI ZA MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI

- JINA LA MZAZI /MLEZI……
- KAZI YA MZAZI /MLEZI ……
- ANUANI YA MZAZI /MLEZI ……..
- NAMBA YA SIMU YA MZAZI /MLEZI ……..
- ANAKOISHI KITONGOJI ……KIJIJI ……KATA ……WILAYA …… MKOA ……..
- NAMBA YA SIMU YA JIRANI YAKO ……..

C:KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA

Mimi ……kidato …….. mwaka …….nimesoma na kuelewa maelekezo yote.Nakubali kuipokea nafasi hii niliyopewa.Nathibitisha wazi kwamba nimepokea maagizo bila kulazimishwana naahidi kuyazingatia

Tarehe …… Saini ……..

D: **KUKUBALI SHERIA ZA SHULE**

MWANAFUNZI:

Mimi …… Nimesoma na kuzielewa sheria za shule na naahidi kwamba nitazizingatia na kutii masharti,sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu wote wa shule

Tarehe …….. Saini …….

MZAZI

Jina …….. Saini …….. Tarehe ……..

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENT
BUSEGA DISRICT MASANZA SECONDARY SHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed **by Medical officer only**

Name of student …… Age……

(To be completed by a government medical officer) : I have examined the above named student and consider that he/she is fit / unfit for a full time students:-

i) Eyesight…….
ii) Hearing ……..
iii) Speech ……..
iv) Limbs ……
v) Venereal ……..
vi) Leprosy ……
vii) Epilepsy ……
viii) Neurosis ……..
ix) Other serious diseases eg Athma ……..
x) Stool examination……
xi) T.B test …….
xii) HIV test……..
xiii) Pregnancy Test …….

Additional information or any other physical, mental hereditary or infections diseases

……

(Please state nature of treatment)

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above mentioned student has been examined and found him/her to be fit/unfit to persue further education.(delete whichever not needed)

Name …… Signature ……..

DESIGNATION …….. STATION …….

Date ……

Official stamp

NB: Fomu hii lazima ijazwe na Daktari katika Hospitali inayotambulika na serikali.